



USHAURI WA SERA

Shughuli za Nje 2023-2

Sera: Uondoaji wa Ombi la BRC Lililotelikezwa au Lisilokamilika

Tarehe ya Kuanza: Jumapili, 1 Oktoba 2023

Kiungo cha Sera: <https://www.mass.gov/doc/abandoned-or-incomplete-brc-request-removals-policyswahili/download>

MUHTASARI

Ili kuhakikisha kuwa orodha ya maombi yanayosubiri Ukaguzi wa Rekodi za Historia (BRC) ni ya sasa na Idara ya Elimu na Utunzaji wa Mapema (EEC) haifanyi ukaguzi wa rekodi za historia kwa wateuliwa ambao wamechukuliwa alama za vidole baada ya muda wa fomu yao ya idhini ya BRC kuisha, EEC itakuwa ikiondoa maombi ya BRC yaliyotelekezwa au ambayo hayajakamilika kwenye Tovuti ya Mpango wa Kielekezi cha BRC baada ya miezi minne.

Sera hii itaathiri waombaji wapya pekee walio na maombi ya BRC:

- ambayo ni zaidi ya miezi minne, na
- ambapo mwombaji hakupanga miadi ya kuchukuliwa alama za vidole au kutoa alama za vidole.

Maombi ya kusasisha BRC ya wafanyakazi wa mpango waliopo hayataathiriwa kwa sasa.

MATUMIZI

Sera hii inatumika kwa mipango yote ua EEC yenye leseni, iliyoidhinishwa, au iliyofadhiliwa.

SASISHO MUHIMU

- Sera Iliyosasishwa
 - EEC inapunguza rekodi ya matukio kutoka mwaka mmoja hadi miezi minne wakati ECC itaondoa maombi ya BRC yaliyotelekezwa au ambayo hayajakamilika katika Tovuti ya Mpango wa Kielekezi cha BRC.
 - Kuanzia Agosti 2023, mipango yote ya EEC yenye leseni, iliyoidhinishwa, au iliyofadhiliwa inatumia Tovuti ya Mpango wa Kielekezi cha BRC kwa mchakato wa BRC. Kwa hiyo, sera hii huathiri aina zote za mpango.

RASILIMALI

Iwapo wewe au wafanyakazi wako mna maswali kuhusu sera hii au mnahitaji usaidizi wa ziada, tafadhalii wasiliana na Kituo cha Mawasiliano cha EEC katika 617-988-7841.

HAITUMIKI

Sera hii inachukua nafasi ya sera ya EEC ya kuondoa maombi ya BRC yaliyotelekezwa au ambayo hayajakamilika kwenye Tovuti ya Mpango wa Kielekezi cha BRC baada ya mwaka mmoja, iliyotolewa tarehe 29 Agosti 2022.